

TOLEO LA. 10

Jarida la *Ni Magufuli Tena*

2020 - 2025

ALIAHIDI | AMETEKELEZA | APEWE TENA 5 | 9 SEPTEMBER, 2020



**GEITA WAAMUA
NI MAGUFULI TENA,
MITANOTENA!**

Limeandaliwa na **TEAM MAGUFULI TENA**



RAIS MAGUFULI KUSHUSHA NEEMA KWA WACHIMBAJI WADOGO

Na Mwandishi Wetu - **GEITA**

Mgombea Urais wa Chama cha Mapinduzi (CCM) na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. John Pombe Magufuli amesema ikiwa atachaguliwa kwa kipindi cha miaka mitano mingine, ataongeza zaidi maeneo ya wachimbaji wadogo na kuwapatia ujuzi zaidi na teknolojia rahisi ili wafanye kazi zao kwa tija. Rais Magufuli ametoa ahadi hiyo leo wakati wa mkutano mkubwa wa kampeni uliofanyika katika uwanja wa Kalangala mjini Geita.

"Mwaka 2016 wachimbaji wadogo waliuza dhahabu iliyowezesha Serikali ilipata mrabaha wa shilingi bilioni 1.2 ila baada ya kuanza kuchukua hatua wachimbaji wadogo waliuza kilo Dhahabu yenye thamani ya shilingi bilioni 337.5 na kutoa mrabaha wenye thamani ya shilingi bilioni 22.5," ameeleza Rais Dkt. Magufuli.

Kwa upande wa wachimbaji wakubwa amesema kuwa waliuza dhahabu zenye thamani ya dola za marekani milioni 449.8 sawa na shilingi trilioni 2.2. Aidha mwaka 2016 wachimbaji wakubwa waliuza dhahabu zilizowezesha kupatikana kwa shilingi trilioni 1.4 na kutoa mrabaha kwa Serikali kiasi cha bilioni 53.81. Ameongeza kuwa Mei 2019, wachimbaji wakubwa walichimba dhahabu yenye thamani ya shilingi trilioni 2.2 na kutoa mrabaha kwa Serikali kwa shilingi bilioni 130.64.

Kwa upande wake, Mgombea Ubunge wa jimbo la Bukombe kwa tiketi ya CCM ambaye pia ni Waziri wa Madini Doto Biteko amesema kuwa mazingira bora na wezeshi yaliyowekwa na Serikali ya Awamu ya Tano katika Sekta ya Madini, yamesababisha kuongezeka kwa wachimbaji wadogo wa madini wenye leseni kutoka 300 mwaka 2015 hadi 1510 mwaka 2020.

Amesema kuwa kutokana na mafanikio yaliyofikiwa katika kipindi cha Serikali ya Awamu ya Tano, Mawaziri wa Madini kutoka nchi saba wameomba kuja kujifunza namna Tanzania inavyosimamia Sekta hiyo. Dhamira ya Serikali ya Awamu ya Tano kusiimamia Sekta ya Madini kikamilifu kumewezesha mapato yake kuongezeka kwa mapato yatoanayo na Sekta hii na hivyo kuchangia katika kukuza uchumi na ustawi wa wananchi.



VIONGOZI WA DINI WAENDELEA KUBARIKI KAMPENI ZA MAGUFULI

Na Mwandishi Wetu

Kama ambavyo amekuwa akiamini na kumshirikisha Mungu katika kila jambo analolifanya, Viongozi wa dini nao wameendelea kumuomba na kumshukuru Mungu kwa kumleta Rais Dkt. John Pombe Magufuli kuwa Kiongozi wa nchi na kuomba Mwenyezi Mungu amsaidie kushinda katika kampeni ya nafasi ya Urais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Viongozi hao wa Dini wamefanya maombi hayo leo kabla ya kuanza kwa mkutano wa kampeni uliofanyika katika Uwanja wa Kalangalala, Geita Mjini na kuhudhuriwa maelefu ya wananchi wa Geita pamoja na wagombea wa Ubunge na Udiwani katika Majimbo na Kata Mkoani huko.

“Tunamshukuru Mungu kwa namna alivyojibu maombi na kutupatia kiongozi huyu, tunaomba utujalie tuchague kiongozi mcha Mungu, mwadilifu na mzalendo ambaye ataendeleaza kazi ya kuwatumikia watu wako na kufanya kazi kwa uadilifu,” alisikika Askofu Mkuu, Mussa Magesela wa Kanisa la Africa Inland Church (AIC) Geita katika sehemu ya maombi yake.

Katika maombi hayo, Askofu Magesela aliongeza: “Tunakemea kila hila za shetani dhidi ya mchakato huu wa kampeni za uchaguzi wa mwaka 2020.”

Kwa upande wake, Sheikh wa Mkoa wa Geita, Alhaji Yusufu Kabaju, aliwaombea wataanzania busara na hekima ili waweze kuchagua viongozi waadilifu na watakaowaletea maendeleo.

Tangu Rais Magufuli aanze kampeni za kugombea nafasi ya Urais kwa miaka mitano mingine, viongozi mbalimbali wa Dini wamekuwa wakifanya maombi na dua kumuomba heri kwa Mwenyezi Mungu ili amlinde katika kampeni zake na aendeleo kufanya kazi ya kuwatumikia wataanzania huku akimtanguliza Mungu.



RAIS MAGUFULI AAHIDI NEEMA YA MAJI KATIKA MIJI 28 GEITA

Na Mwandishi Wetu - **GEITA**

Serikali ya Awamu ya Tano ni Serikali ya KUAHIDI NA KUTEKELEZA. Hivi ndivyo miji 28 katika mkoa wa Geita inavyosubiri kunufaika na miradi ya maji itakayotekelezwa na Serikali ya Awamu ya Tano mara tu baada ya wananchi watakapoichagua kwa kishindo Oktoba 28, 2020.

Akiomba kura kwa wananchi wa Geita mjini na vitongoji vyake wakati wa mkutano wa hadhara katika uwanja wa Kalangalala mjini humo, Mgombea Urais wa Chama cha Mapinduzi (CCM) na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. John Pombe Magufuli amesema kuwa kiasi cha shilingi bilioni 130 kimetengwa kwa ajili ya kuwezesha upatikanaji wa maji katika miji 28 nchini.

“Kwa kweli Geita mmefanya makubwa, sikutegemea mngejaa hivi, Geita hongereni sana, naendelea kuwa na deni kwenu.

Mkinichagua nitaendelea kumtanguliza Mungu katika kuhakikisha tunatekeleza kikamilifu miradi hii ya maendeleo ikiwemo barabara na maji.

“Mradi mwingine wa maji wenye thamani ya shilingi bilioni 36.5 unanufaisha maeneo ya Nyamtukuza, Chopologo, Muharamba, Ruhuhu na Nyakagomba” ameeleza Rais Dkt. Magufuli.

Kwa upande wa barabara, Serikali itajenga kwa kiwango cha lami barabara ya Geita-Bukoli hadi Kahama yenye urefu wa kilomita 107 ili kuchochea shughuli za kiu-chumi na ustawi wa wananchi.

Kwa upande wa Sekta ya Afya amesema kuwa ujenzi wa hospitali ya rufaa ya mkoa utaendelezwa na pia hospitali za wilaya mbili zimejengwa na watumishi 192 wamepelekwa katika mkoa wa Geita.



SERIKALI YA CCM KUNUNUA MELI TANO ZA UVUVI UKANDA WA PWANI

Na Mwandishi Wetu - **Nakungurukuru, LINDI**

Mgombea Mwenza wa Urais kupitia Chama Cha Mapinduzi (CCM), Mhe. Samia Suluhu Hassan, amesema Serikali imepanga kununua meli tano kubwa za uvuvi zitakazotumika katika ukanda wa pwani, lengo likiwa ni kutoa fursa zaidi ya ajira kwa vijana na kuwawezesha watazania kunufaika na rasilimali za Bahari katika ukanda huo.

Ununuzi wa meli hizo utakwenda sambamba na ujenzi wa bandari ya uvuvi ambayo meli zote zitakazovua kwenye eneo la bahari ya Tanzania zitatakiwa kutia nanga ili kuwe na mapato stahiki ya Serikali.

Akizungumza na wananchi wa Nangulukulu, mkoa wa Lindi, wakati akiwa njiani kuelekea Mtwara, Mhe. Samia amesema hatua hiyo itasaidia kuondoa wizi uliokuwa ukifanywa na meli za uvuvi zinazovua samaki ukanda wa bahari ya Tanzania.

"Tutanunua meli tano za uvuvi ambazo tutawafundisha vijana wetu kuvua samaki katika eneo letu la bahari, pia tutajenga bandari ya uvuvi ambayo meli zote za uvuvi zitatia nanga na tutafahamu kiwango cha samaki walichovua ili tupate mapato yetu badala ya kuibiwa," ameeleza Mgombea Mwenza.

Aliwaomba wakazi hao kumchagua Dkt. John Pombe Magufuli ili kukamilisha mambo yote hayo yanayolenga kujenga uchumi wa watu wa Mikoa ya kanda ya Kusini. "Chama pekee kilichojipanga kuwaletea watazania maendeleo ni CCM. Tutaleta maendeleo kwa vizazi vya leo na vinavyokuja," Mama Samia amebainisha.

Aidha, akizungumza na wananchi wa Mchinga, Mhe. Samia amewaeleza kuwa Serikali inatambua changamoto ya maji katika eneo hilo na kwamba baada ya miaka miwili ijayo shida ya maji katika eneo hilo itakuwa imetatuliwa.

Kuhusu shida ya kivuko kutoka Mchinga moja hadi Mchinga mbili, Mama Samia amesema atatuma wataalamu wa vivuko kuangalia eneo hilo ili changamoto hiyo iweze kutatuliwa.

Kwa upande wake Rais Mstaafu wa Awamu ya Nne, Mhe. Jakaya Mrisho Kikwete, amesema wananchi wa Lindi wasubiri neema kutokana na ujio wa ujenzi wa kiwanda cha kuchakata gesi Likong'o.

Amesema kiwanda hicho kitakuwa na thamani ya dola bilioni 30 ambapo pia mji wa kisasa utajengwa na wananchi kunufaikaikiwemo kupataba ajira. "Asiwadanganye mtu, maendeleo yanapatikana. Hakuna wa kubabaika wala kubabaishwa. CCM ni Chama chenye viongozi makini," alieleza.



5 KALI ZA MAGUFULI MKOANI GEITA

01

Kutokana na hatua tulizochukua kwenye madini mkoani Geita, uuzaji wa madini ya wachimbaji wadogo umeongezeka kutoka shilingi bilioni 22.5 na kutoa mrabaha kwa Serikali shilingi bilioni 1.2 kwa mwaka 2016 wakati mwaka 2019 wachimbaji hao waliuza madini yenye thamani ya shilingi bilioni 375.5 na kutoa mrabaha wa shilingi bilioni 22.5.

02

Idadi ya watu Katoro na Buselele ni kubwa sana hivyo nasema wazi kuwa ndani ya mwaka wa kwanza mkituchagua, nataka wabunge waandae mkakati wa kutengeneza wilayana mpya hapa Katoro.

03

Tunatekeleza mradi mkubwa wa maji wenye thamani ya shilingi bilioni 36.5 na tunaendelea na miradi mingine midogo midogo. Aidha mji wa Geita umepangwa katika mradi mkubwa wa miji 28 utakaopatiwa maji na ume-tengewa shilingi bilioni 130.

04

Katika miaka mitano inayokuja tutatengeneza barabara za lami nyingi zaidi hapa Geita, mtakapotuchagua tume-panga kujenga barabara ya kutoka Geita kwenda Kahama kwa kiwango cha lami.

05

Natoa wito kwa watu wengine duniani waje wajifunze Tanzania jinsi Mungu anavyoweza kufanya maajabu hata katika magonjwa makubwa yaliyoshindikana.



BUKOMBE WAAHIDI KURA ZA KISHINDO KWA MAGUFULI

Na Mwandishi Wetu

Wananchi wa Jimbo la Bukombe wamemuahidi kura za kishindo mgombea Urais wa Chama cha Mapinduzi (CCM) na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. John Pombe Magufuli katika Uchaguzi Mkuu wa Oktoba 28, 2020.

Akizungumza kwa niaba ya wananchi hao, mgombea Ubunge wa jimbo la Buombe ambae pia ni Waziri wa Madini, Mhe. Doto Biteko amesema kuwa wananchi wa jimbo hilo wamenufaika na miradi mbalimbali ukiwemomradi wa maji wenye thamani ya shilingi bilioni tano.

“Rais Magufuli amewezesha jimbo letu la Bukombe kuwa na barabara za lami na miradi mingine ya maendeleo ikiwemo ya afya, elimu, maji na mindombinu hivyo wananchi wa Bukombe wanasema watampigia kura zote za ndiyo kutokana na kazi kubwa aliyowafanyia wananchi,” ameeleza Biteko.

Akifafanua zaidi, Mhe. Biteko amesema kuwa wananchi wa Bukombe wameukubali uongozi wa na utekelezaji wa Serikali ya Awamu ya Tano chini ya Rais Magufuli hivyo wana kazi moja tu kuhakikisha CCM inashinda kwa kishindo katika nafasi zote.

Mgombea Urais wa Chama cha Mapinduzi (CCM) na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. John Pombe Magufuli anaendelea na Kampeni zake katika mkoa wa Geita kuomba ridhaa ya wananchi kuchaguliwa kwa awamu ya pili ya kipindi cha miaka mitano ijayo.

Jarida la Ni Magufuli Tena

2020 - 2025



Limeandaliwa na **TEAM MAGUFULI TENA**